

Maziwa yatajwa tiba ya uzee, vidonda vya tumbo

Na Dege Masoli, TANGA

UNYWAJI maziwa umeelezwa kuwa na faida nyingi ikiwamo kuzuia uzee kabla ya wakati, ngozi kutokukunjamana na kuzuia meno kuuma hadi kufikia hatua ya kung'oa.

Kutokana na faida hizo, Watanzania wametakiwa kutilia mkazo unywaji maziwa ili kupata manufaa hayo pamoja na ulinzi wa mwili dhidi ya maradhi.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja wa Vyanzo vya Maziwa kutoka kiwanda cha Tanga (Tanga Fresh), Nadomana Nyanga, baada ya maandishi wa habari kutembelea kiwandani hapo kwa lengo la kujionea mafanikio yaliyofikiwa katika kuboresha ubora wa huduma ya maziwa.

Nyanga alisema utafiti unaonyesha unywaji wa maziwa ni njia pekee inayoweza kusaidia mtu kuepukana na baa-

dhi ya madhara yanayotokana na jamu kukosa utamaduni wa kutumia maziwa.

Alisema unywaji maziwa unasaidia kuondoa uzee, ngozi kukunjama kwa binadamu, kuzuia tatizo la meno kuuma na kusababisha hata hatua ya kung'olewa na kwamba njia kuu ni pamoja na kunywa maziwa bora ambayo hayajachanganywa na maji. Nyanga alisema endapo Watanzania watajiwekea utamaduni wa kunywa maziwa, matatizo yote hayo watayaepuka kutokana na ukweli kuwa yana virutubisho vingi ambavyo hufanya mwili uongeze kinga muda wote.

Aliongeza kuwa wakiwa wataalamu wa maziwa, wanajitahidi kuwahamasisha wananchi watumie maziwa kama kinywaji cha kawaida ili kuongeza kinga ya mwili na hatimaye kuwa na afya njema.

Kwa upande wake, mtaalamu wa mbuzi wa maziwa kutoka kituo cha utafiti wa malisho ya mifugo (Taliri) mkoani

Tanga, Ayubu Kambadu,

alisema asilimia kubwa ya watu wamekuwa wakifika kituoni hapo wakisema kuwa unywaji wa maziwa ya mbuzi umelowa ukiwasaidia kwa kiwango kikubwa kutibu matatizo ya vidonda vya tumbo hali inayosababisha kufanya utafiti kwa kina. Mtaalamu huyo alisema mbuzi wanaopata malisho mazuri na chakula bora wanarwezo wa kutoa maziwa lita mbili kwa siku na maziwa yake yana virutubisho vingi vinavyoweza kumsaidia binadamu aweze kuongeza kinga ya mwili na kuepukana na magonjwa yasiyo ya kuambukizwa.

Aliongeza kuwa wamekuwa wakizalisha mbegu bora za mbuzi wa maziwa na kwamba kwa sasa wamejipanga kuhakikisha wanaongeza mbegu bora ili kuwawezesha wananchi kununua kwa wingi na hatimaye kupata tiba ya tatizo hilo.

Vijana kunufaiika mtandao wa UVUVI

Na Mwandishi Wetu

VIJANA kutoka mikoa 13 ya Tanzania Bara na Visiwani watanufaika na mtandao wa vijana unaojihusisha na shughuli za uvuvi na mifugo.

Lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo kutawasaidia vijana nchini kujajiri moja kwa moja kupitia mtandao huo wa uvuvi na mifugo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mtandao huo, uhoftanyika jijini Arusha, Rais wa Mtandao huo, Laban Boaz, alisema vijana chini ya miaka 35, kutoka mikoa hivyo watanufaika na mtandao huo kwa kufundishwa mbinu bora za kisasa za ufugaji.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo, ni kuhamasisha vijana

nchini, kujajiri katika sekta ya mifugo na uvuvi kwa kutumia njia ya kisasa ambazo zitasaaidia kuongeza uzalishaji mali na ajira kwa vijana.

Alisema walianzisha mtandao huo, tsaida ya kuona kuna mwanja wa kimaendeleo kati ya wazee na vijana.

"Mtandao huu utasaidia kuwapa ujuzi na maarifa vijana namina ya kufuga kisasa na vijana waliopo vijijini ambao hawakupata maarifa haya lengo la mtandao huu ni kuwanufaisha vijana wote," alisema Laban. Alisema mtandao huo ulianzishwa jijini Dar es Salaam mwaka 2017, lengo likiwa ni kupanua wigo kwa vijana nchini.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde, alisema mtandao huo ni juhudi za muda mrefu zilizofanywa na Umoja wa

Afrika kupitia mradi wa kuendeleza rasilimali za wanyama (AU-IBAR).

Alisema mtandao huo, umewashiriki-sha vijana wanaojihusisha na kazi tofauti katika mnyororo wa thamani ya mifugo, samaki, kuku na nguruwe na vijana hao, kupitia mtandao huo watawekwa pamoja na kufanya kazi ya mnyororo wa thamani.

Nandonde alisema serikali itaendelea kushirikiana na mtandao huo, kuwafikia vijana ili waitumie fursa hiyo ipasavyo.

Makamu wa Rais wa Mtandao huo, Veronica Lyambiko, alisema wamefikia hatua ya kuanzisha mtandao huo, kwa kuwa vijana wengi nchini wanakabilwa na tatizo la ajira.

Alisema, kupitia mtandao huo, idadi ya vijana wataingia na kuwafikia vijana waliopo vijijini.